



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



**TAARIFA YA MATOKEO YA MTHANI WA KIDATO CHA SITA
(ACSEE) ULIOFANYIKA MEI 2022**

IMETOLEWA NA :

KAIMU KATIBU MTENDAJI

05 JULAI, 2022

TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) ULIOFANYIKA MEI, 2022

1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **147** uliofanyika tarehe **05 Julai 2022** katika ukumbi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) - Zanzibar, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita (**ACSEE**) uliofanyika tarehe **09 - 27 Mei, 2022**.

2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

2.1 Watahiniwa wote

Jumla ya watahiniwa **95,826** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei, 2022 wakiwemo wasichana **41,517 (43.33%)** na wavulana **54,309 (56.67%)**. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa wa Shule walikuwa **85,414** na watahiniwa wa kujitegemea walikuwa ni **10,412**.

Kati ya watahiniwa **95,826** waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei, 2022, watahiniwa **94,456** sawa na asilimia **98.57** walifanya mtihani na watahiniwa **1,370** sawa na asilimia **1.43** hawakufanya mtihani kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za Ugonjwa na Utoro.

2.2 Watahiniwa wa Shule

Kwa Watahiniwa wa Shule, kati ya watahiniwa **85,414** waliosajiliwa, watahiniwa **84,870** sawa na asilimia **99.36** walifanya mtihani ambapo wasichana walikuwa **37,468 (99.54%)** na wavulana **47,402 (99.23%)**. Watahiniwa **544 (0.64%)** hawakufanya mtihani.

2.3 Watahiniwa wa Kujitegemea

Kwa Watahiniwa wa Kujitegemea, kati ya watahiniwa **10,412** waliosajiliwa, watahiniwa **9,586** sawa na asilimia **92.07** walifanya mtihani na watahiniwa **826** sawa na asilimia **7.93** hawakufanya mtihani.

3.0 MATOKEO YA MTIHANI

3.1 Watahiniwa Wote

Jumla ya watahiniwa **93,136** sawa na asilimia **98.97** ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei, 2022 wamefaulu. Wasichana waliofaulu ni **40,907** sawa na asilimia **99.51** wakati wavulana waliofaulu ni **52,229** sawa na asilimia **98.55**. Mwaka 2021 watahiniwa waliofaulu walikuwa **87,043** sawa na asilimia **99.06**.

3.2 Watahiniwa wa Shule

Watahiniwa wa Shule waliofaulu ni **84,404** sawa na asilimia **99.87** ya waliofanya mtihani. Wasichana waliofaulu ni **37,384** sawa na asilimia **99.91** na wavulana ni **47,020** sawa na asilimia **99.83**. Mwaka 2021 Watahiniwa **79,596** sawa na asilimia **99.62** ya Watahiniwa wa Shule walifaulu mtihani huo.

3.3 Watahiniwa wa Kujitegemea

Idadi ya Watahiniwa wa Kujitegemea waliofaulu mtihani ni **8,732** sawa na asilimia **91.11**. Mwaka 2021, Watahiniwa wa Kujitegemea **7,447** sawa na asilimia **93.45** walifaulu mtihani huo.

4.0 UBORA WA UFAULU

Ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata Watahiniwa wa Shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **83,877** sawa na asilimia **99.24** wamefaulu katika **Daraja la I hadi III** wakiwemo wasichana **37,170** sawa na asilimia **99.34** na wavulana **46,707** sawa na asilimia **99.16**.

Jedwali lifuatalo linaonesha ufaulu kwa kila Daraja kwa Watahiniwa wa Shule na kwa Jinsi:

Madaraja ya ufaulu	Wavulana		Wasichana		Jumla	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
I	15,623	33.17	11,674	31.20	27,297	32.30
II	22,405	47.57	17,753	47.45	40,158	47.51
III	8,679	18.43	7,743	20.69	16,422	19.43
I – III	46,707	99.16	37,170	99.34	83,877	99.24
IV	313	0.66	214	0.57	527	0.62
I – IV	47,020	99.83	37,384	99.91	84,404	99.87
O	82	0.17	32	0.09	114	0.13

5.0 UFAULU WA MASOMO KWA WATAHINIWA WA SHULE

Takwimu za ufaulu kwa watahiniwa wa Shule wa Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) Mei, 2022 zinaonesha kuwa ufaulu katika masomo ya, **History, English Language, French Language, Arabic Language, Physics, Chemistry, Biology, Agriculture, Advanced Mathematics, Economics, Accountancy** na **Food and Human Nutrition** umepanda ikilinganishwa na mwaka 2021.

Ufaulu katika somo la **Commerce** ni asilimia **99.85** sawa na mwaka 2021. Ufaulu katika somo la **Kiswahili** ni asilimia **100** sawa na ufaulu wa somo hilo kwa mwaka 2021. Aidha, ufaulu katika masomo ya **General Studies**,

Geography, Basic Applied Mathematics na Computer Science umeshuka ikilinganishwa na mwaka 2021. Mchanganuo wa ufaulu kwa kila somo umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

NA.	SOMO	2021	2022
		UFAULU (%)	UFAULU (%)
1.	GENERAL STUDIES	98.05	97.12
2.	HISTORY	99.68	99.90
3.	GEOGRAPHY	99.92	99.87
4.	KISWAHILI	100.00	100.00
5.	ENGLISH LANGUAGE	99.69	99.94
6.	FRENCH LANGUAGE	97.28	98.09
7.	ARABIC LANGUAGE	75.00	93.61
8.	PHYSICS	93.60	97.48
9.	CHEMISTRY	94.81	97.48
10.	BIOLOGY	96.81	99.26
11.	AGRICULTURE	95.16	100.00
12.	COMPUTER SCIENCE	60.52	22.15
13.	BASIC APPLIED MATHEMATICS	60.85	58.66
14.	ADVANCED MATHEMATICS	93.49	97.89
15.	ECONOMICS	99.27	99.73
16.	COMMERCE	99.85	99.85
17.	ACCOUNTANCY	97.71	99.93
18.	FOOD AND HUMAN NUTRITION	98.29	99.66

6.0 SHULE KUMI (10) BORA KITAIFA

Ubora wa shule umepangwa kwa kutumia kigezo cha **Wastani wa Pointi (Grade Point Average – GPA)** kwa ufaulu wa shule kimasomo na kimadaraja. Mchanganuo wa Shule zilizofanya vizuri zaidi ni kama ifuatavyo:

NA.	JINA LA SHULE	IDADI YA WATAHINIWA	MKOA	UMILIKI
1.	KEMEBOS	34	KAGERA	BINAFSI
2.	KISIMIRI	94	ARUSHA	SERIKALI
3.	TABORA BOYS'	156	TABORA	SERIKALI
4.	TABORA GIRLS'	140	TABORA	SERIKALI
5.	AHMES	189	PWANI	BINAFSI
6.	DAREDA	116	MANYARA	SERIKALI
7.	NYAISHOZI	47	KAGERA	BINAFSI
8.	MZUMBE	166	MOROGORO	SERIKALI
9.	MKINDI	57	TANGA	SERIKALI
10.	ZIBA	74	TABORA	SERIKALI

7.0 WATAHINIWA WALIOFANYA VIZURI ZAIDI KITAIFA

Watahiniwa waliofanya vizuri zaidi kitaifa wamepatikana kwa kulinganisha jumla ya pointi kwenye masomo ya **tahasusi** (combination) pamoja na wastani wa alama za jumla walizopata.

7.1 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	CATHERINE ALPHONCE MWAKASEGE	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
2.	LUCY E MAGASHI	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
3.	MUHEWA CHARLES KAMANDO	M	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
4.	MINAEL SIMON MGONJA	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
5.	NORAH ELIAZA KIDJOUT	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
6.	JENNIFER MARTIN CHUWA	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
7.	PAULINE ILDEPHONCE MABAMBA	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
8.	RACHEL JOACHIM MOSHY	F	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
9.	KULWA MBIZO ELIAS	M	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
10.	OSCAR ELIAKIM MARABE	M	TABORA BOYS'	TABORA	PCB

(a) Wasichana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	CATHERINE ALPHONCE MWAKASEGE	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
2.	LUCY E MAGASHI	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
3.	MINAEL SIMON MGONJA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
4.	NORAH ELIAZA KIDJOUT	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
5.	JENNIFER MARTIN CHUWA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
6.	PAULINE ILDEPHONCE MABAMBA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
7.	RACHEL JOACHIM MOSHY	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCM
8.	DINA STEVEN NGIGA	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	PCB
9.	JUDITH KABELINDE BENEDICTOR	KILAKALA	MOROGORO	PCM
10.	JULITHA FLORIAN SILANGWA	BRIGHT FUTURE GIRLS	DAR ES SALAAM	PCM

(b) Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Sayansi

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	MUHEWA CHARLES KAMANDO	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
2.	KULWA MBIZO ELIAS	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
3.	OSCAR ELIAKIM MARABE	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
4.	BARAKA HEZRON NYOTA	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
5.	DON MWAKATOGA	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
6.	PWALI JOSHUA NJOGELA	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
7.	ALBERT TASU MASHAURI	MZUMBE	MOROGORO	PCB
8.	ZAFRULLAH ABDUL-RAHMAN MOHAMMED	TABORA BOYS'	TABORA	PCB
9.	PHILIPO ANTIPAS NG'ELESHI	WARI	KILIMANJARO	PCB
10.	KENNEDY CLETUS MCHARO	WARI	KILIMANJARO	PCM

7.2 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	HAMZA MASUDI NGOSSE	M	SONGEA BOYS'	RUVUMA	HGK
2.	CHARITE HIMA CHONZA	F	ZAKIA MEGHJI	GEITA	EGM
3.	ZILABHELA KAHILIMA KOMBWEY	F	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
4.	MEBO LEO MGAYA	F	AHMES	PWANI	EGM
5.	GILEAD P GWASELYA	M	TUKUYU	MBEYA	EGM
6.	ALBERT VENANCE BONIPHACE	M	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
7.	ABDALLAH SALUM MTAWANYIKA	M	KEMEBOS	KAGERA	HGL
8.	WINIFRIDA J SUGOYA	F	AHMES	PWANI	HKL
9.	HASSAN KURWA BURUHANI	M	MUSOMA	MARA	HGL
10.	ERICK GODVIN MLAY	M	DAREDA	MANYARA	HGL

(a) Wasichana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	CHARITE HIMA CHONZA	ZAKIA MEGHJI	GEITA	EGM
2.	ZILABHELA KAHILIMA KOMBWEY	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
3.	MEBO LEO MGAYA	AHMES	PWANI	EGM
4.	WINIFRIDA J SUGOYA	AHMES	PWANI	HKL
5.	GRACE AMOSI FILEMONI	DAREDA	MANYARA	HKL
6.	NAHYA SAID AHMED	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	EGM
7.	LISA FRANCIS ASSEY	ST.MARY'S MAZINDE JUU	TANGA	EGM
8.	SHAKLINA OMARY MKANDAMA	AHMES	PWANI	EGM
9.	MARY K HIZA	AHMES	PWANI	HKL
10.	CLEMENTINA FAUSTIN GEAY	DAREDA	MANYARA	HKL

(b) Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Lugha na Sanaa

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	HAMZA MASUDI NGOSSE	SONGEA BOYS'	RUVUMA	HGK
2.	GILEAD P GWASELYA	TUKUYU	MBEYA	EGM
3.	ALBERT VENANCE BONIPHACE	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
4.	ABDALLAH SALUM MTAWANYIKA	KEMEBOS	KAGERA	HGL
5.	HASSAN KURWA BURUHANI	MUSOMA	MARA	HGL
6.	ERICK GODVIN MLAY	DAREDA	MANYARA	HGL
7.	VINCENT RESPIGI TEMBA	KISIMIRI	ARUSHA	HKL
8.	INNOCENT PHILEMONI ELIKUNDA	DAREDA	MANYARA	HKL
9.	ELIBARIKI EMANUEL AMMI	DAREDA	MANYARA	HKL
10.	ABRAHAMANI K MUSSI	DAREDA	MANYARA	HKL

7.3 Watahiniwa Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	JINSI	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	ESTHER PAUL CHAMA	F	KEMEBOS	KAGERA	ECA
2.	DORCAS MGENDI CHACHA	F	ARUSHA	ARUSHA	ECA
3.	SULTAN NASORO MOHAMED	M	ISTIQAAMA TANGA ISLAMIC	TANGA	ECA
4.	NASRA ALI OMAR	F	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	ECA
5.	GLADNESS ROMAN SWAI	F	CANOSSA	DAR ES SALAAM	ECA
6.	GLADYS OCTAVIAN AMLIMA	F	ST. CHRISTINA GIRLS'	TANGA	ECA
7.	ASYA RASHID ALLY	F	SHAABAN ROBERT	DAR ES SALAAM	ECA
8.	TECLA SAMUEL MSHOTE	F	TUSIIME	DAR ES SALAAM	ECA
9.	AISHA H KILONDA	F	TAMBAZA	DAR ES SALAAM	ECA
10.	EDNA EMANUEL URIO	F	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA

(a) Wasichana kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	ESTHER PAUL CHAMA	KEMEBOS	KAGERA	ECA
2.	DORCAS MGENDI CHACHA	ARUSHA	ARUSHA	ECA
3.	NASRA ALI OMAR	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	ECA
4.	GLADNESS ROMAN SWAI	CANOSSA	DAR ES SALAAM	ECA
5.	GLADYS OCTAVIAN AMLIMA	ST. CHRISTINA GIRLS'	TANGA	ECA
6.	ASYA RASHID ALLY	SHAABAN ROBERT	DAR ES SALAAM	ECA
7.	TECLA SAMUEL MSHOTE	TUSIIME	DAR ES SALAAM	ECA
8.	AISHA H KILONDA	TAMBAZA	DAR ES SALAAM	ECA
9.	EDNA EMANUEL URIO	WERUWERU	KILIMANJARO	ECA
10.	ESTHER S MALEBETO	BUKONGO	MWANZA	ECA

(b) Wavulana Kumi (10) Bora Kitaifa kwa Masomo ya Biashara

NA.	JINA	SHULE	MKOA	MCHEPUO
1.	SULTAN NASORO MOHAMED	ISTIQAAMA TANGA ISLAMIC	TANGA	ECA
2.	YUSSUF OMARY KHAMISI	TAMBAZA	DAR ES SALAAM	ECA
3.	DENIS EMMANUEL MATEMU	SENGEREMA	MWANZA	ECA
4.	MANSURY MBARAKA MTANDAMO	UMBWE	KILIMANJARO	ECA
5.	RICHARD MATHIAS RICHARD	KEMEBOS	KAGERA	ECA
6.	WILLIAM RICHARD MAIKA	ROSMINI	TANGA	ECA
7.	IDRISA ALI SHAABAN	ZANZIBAR COMMERCIAL	MJINI MAGHARIBI	ECA
8.	ALLY M KONDO	BAOBAB	PWANI	ECA
9.	BHIZABHITYO BHIYAKA BHIZABHITYO	KIBAHA	PWANI	ECA
10.	WAZIRI J NGALUYA	KIBAHA	PWANI	ECA

8.0 TATHMINI YA AWALI YA MATOKEO

Ufaulu wa jumla ya Watahiniwa wa Shule katika Mtihani wa Kidato cha Sita 2022 unaonesha kupanda kidogo kwa asilimia **0.25** ambapo mwaka 2021 ufaulu ulikuwa asilimia **99.62** na mwaka 2022 ufaulu ni asilimia **99.87**. Ubora wa ufaulu kwa watahiniwa waliofaulu vizuri katika daraja la I, II na III umeongezeka kwa asilimia **1.31** ukilinganishwa na mwaka 2021. Aidha, ufaulu wa jumla na ubora wa ufaulu wa wasichana kwa mwaka 2022 umezidi kidogo ule wa wavulana kwa asilimia **0.08** na **0.18** mtawalia.

Baraza la Mitihani la Tanzania litafanya uchambuzi wa kina wa matokeo haya kwa kila somo na kutoa machapisho ya uchambuzi huo yatakayowasilishwa kwa wadau wa Elimu, zikiwemo shule zote za Sekondari ya juu ('A' level) nchini kwa lengo la kuwawezesha walimu kutumia taarifa za uchambuzi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

9.0 MATOKEO YA MTIHANI YALIYOZULIWA

Baraza la Mitihani la Tanzania **limezuia** kutoa matokeo ya watahiniwa **21** wa shule ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani kwa baadhi ya masomo. Watahiniwa husika wamepewa fursa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei, 2023, kama watahiniwa wa shule.

10.0 MATOKEO YA MTIHANI YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani la Tanzania limefuta matokeo yote ya watahiniwa 15 waliobainika kufanya udanganyifu katika mtihani. Kati ya watahiniwa hawa, 13 ni watahiniwa wa shule na wawili (02) ni watahiniwa wa kujitegemea.

11.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Majiji nchini, Wakuu wa Shule na Wasimamizi wa Mitihani iliyofanyika Mei, 2022 kwa kuzingatia na kusimamia taratibu za Uendeshaji Mitihani na hivyo kuzuia kwa kiasi kikubwa udanganyifu kufanyika.

12.0 KUANGALIA MATOKEO YA MTIHANI

Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) uliofanyika Mei, 2022 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- <https://matokeo.necta.go.tz>,
- www.necta.go.tz,
- www.tamisemi.go.tz,
- www.tanzania.go.tz

Athumani S. Amasi
KAIMU KATIBU MTENDAJI



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022